Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 5, Issue 1
27th Dhul-Hijjah 1431
3rd December, 2010

FADHLA ZA MWEZI WA MUHARRAM

Yaliyomo

Fadhla Za Mwezi Wa Muharram 1 – 3
Maana Ya 'Ilmu 3
Wajibu Wa Jamaa'ah 3 - 4

FAIDA ZAKE

Na hikma ya upambanuzi huo ('Arafah na 'Ashurah) ni kwamba 'Arafah ni siku iliyo nasibishwa kwa Muhammad yaani saumu yake inahusu Umma wa Muhammad peke yake na siku ya Ashurah ni siku iliyo nasibishwa kwa Nabii Musa (عليه السلام), na Mtume wetu Muhammad ni bora wa Mitume wote (عليهم السلام)

WAJIBU WA KUIFUNGA SIKU HIYO

KWANZA Imepokewa kutoka kwa Jabir bin Samurah (رضي الله عنه) yakwamba alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akiamrisha na kutuhimiza kuifunga siku ya 'Ashura. Ilipofaradhishwa Ramadhani hakuamrisha kufunga na wala hakutukataza.

PILI: Imepokewa kutoka kwa Abu Musa Al-Ash'aree (رضي الله عنه) yakwamba: "Mayahudi walikuwa wakiihisabu siku hiyo ya 'Ashura kuwa ni 'Idd akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم) basi na nyinyi ifungeni".

TATU: Imepokewa na Salama bin Aqwa (رضي الله عنه) yakuwa amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliamrisha mtu mmoja kutoka katika kabila la Aslam yakwamba wawatangazie watu waliokwisha kula wajizuilie kwa mchana ulio bakia na ambaye hajala na aedelee kufunga kwani leo ni siku ya 'Ashura."

NNE: Imepokewa na Rubey bint Mu'aadh ibn Afrah (رضي الله عنها) yakwamba amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipeleka ujumbe asubuhi ya siku ya 'Ashura katika vijiji vya Answar kwamba aliyepambaukiwa hali ya kuwa ni mwenye kula basi ajizuilie mchana uliobakia na aliye pambaukiwa hali yakuwa amefunga basi na aendelee kufunga. Tulikuwa tukifunga baada ya hapo na tukiwafungisha watoto wetu wadogo na tulikuwa tukiwapa vidude vya kuchezea vya sufi akililia mmoja wao chakula tunampa vidude hivyo vya kuchezea mpaka ufike wakati wa kufungua."

KUFUTWA HUKMU HIYO NA KUBAKIA KUWA NI SUNNAH

Imepokewa kutoka kwa Bibi Aisha (رضي الله عنها) yakwamba amesema: "Siku ya 'Ashura ilikuwa ni siku wanayoifunga makureishi wakati wa ujahiliya na Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiifunga alipofika Madina aliifunga na akawaamrisha watu waifunge lakini ilipofaradhishwa saumu ya Ramadhani alisema, '*anayetaka aifunge hiyo Ashura na anayetaka aiwache.*' Amesema Al Baghawi (رحمه الله): "Saumu ya 'Ashura mwanzo kabisa ilikuwa ni faradhi. Baada ya kufaradhishwa saumu ya Ramadhani anaye taka afunge Ashura na anayetaka aiwache. Neno hilo limetokana na 'Aaisha na Abdillah bin Mas'oud na Abdillah bin 'Umar na Jaabir bin Samura (رضي الله عنهم). Amesema al-Haafidh Ibn Hajar katika Fat-hul-Baari: "Huchukuliwa kutokana na hadeeth hizo kwamba saumu hii ilikuwa ni lazima kwa kuthubutu amri ya kuifunga, kisha ikakokotezwa amri ya kuifanya kisha ikazidishwa kukokotezwa kwa ule ulingano wenye kuenea kisha ikazidishwa tena kwa kuamrishwa aliyekula asubuhi ajizuilie kula kisha ikazidishwa tena kwa kuamrisha kina mama wasiwanyonyeshe watoto wao katika siku hiyo.

Na ukishajua kwamba kufika kwa Mtume Madina ilikuwa ni mfungo sita itakuwa kuamrishwa kufunga hiyo 'Ashura ni mwanzo wa Mwaka wa pili na katika huo mwaka wa pili ikafaradhishwa saumu ya mwezi wa Ramadhani. Kwahiyo haikutokea

FADHLA ZA MWEZI WA MUHARRAM

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

kuamrishwa kwa saumu ya Ashura isipokuwa kwa mwaka mmoja kisha likategemezwa jambo la kuifunga saumu hiyo kwa mwenye rai (nguvu za ki-afya) ya kuifunga. Na hivyo hivyo alikufa bwana Mtume (صلى الله عليه وسلم) na haliyakuwa amefunga Ramadhan tisa.

AMRI YA KUWAKHALIFU MAYAHUDI NA MANASWARA

Imepokewa kutoka ibn 'Abbas (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipofika Madina aliwakuta Mayahudi ni wenye kufunga siku ya 'Ashura. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawauliza: *"Ni siku gani hii munayoifunga?"* Wakasema: "Hii ni siku kubwa ambayo Allaah alimuokoa Musa na jamaa zake na akamgharikisha Fir'aun na jamaa zake. Nabii Musa aliifunga kwa kumshukuru Allaah na sisi tunaifunga." Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Basi sisi tuna haki zaidi na ni bora zaidi kwa Musa kuliko nyinyi."* Kwahivyo Mtume aliifunga na akaamrisha watu kuifunga. Na imepokewa tena na Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipoifunga siku ya 'Ashura na akaamrisha watu kuifunga, Maswahaba walisema; "Ewe Mtume wa Allaah! Hii ni siku ambayo Mayahudi na Manaswara wanaitukuza." Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): '*Ukifika mwaka ujao Insha-Allaah tutafunga siku ya tisa.*' Haukufika mwaka ujao Mtume akafariki. Katika mapokezi mengine; '*Nikibakia mpaka mwaka ujao nitafunga siku ya tisa.*'

Amesema ibn Taymiyyah katika kitabu chake *Al-Iqtidhwa;* "ZINGATIA - siku hii ya 'Ashura ni siku bora, saumu yake hufutwa madhambi yake ya mwaka uliopita. Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliifunga na akaamrisha watu waifunge na akapendekeza katika kuifunga siku hiyo. Kisha alipoambiwa nyuma kidogo ya kufa kwake kuwa siku hii Mayahudi na Manaswara wanaitukuza, aliamrisha watu kuwakhalifu hao Mayahudi na Manaswara kwa kuiongezea siku ya tisa na akaazimia kuifunga siku hiyo .Na Amesema Ibn Taymiyyah katika *Fataawa* "Ulipofika mwisho wa Umri wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kumfikia yakwamba Mayahudi wanaifanya siku ya 'Ashura kuwa ni 'Idd, alisema: "*Naapa yakwamba nikiishi mpaka mwaka ujao, nitafunga siku ya tisa kwa ajili ya kuwakhalifu Mayahudi na kutofanana nao katika kuifanya siku hiyo kuwa ni 'Idd.*"

KUNAKILI IKHTILAFU ZA WANAVYUONI KATIKA SAUMU YA SIKU YA 'ASHURA

Wametaja wanavyuoni kwamba saumu ya siku ya 'Ashura iko juu ya daraja tatu;

* Daraja ya kwanza ni kufunga siku tatu , ni siku ya tisa ya kumi na kumi na moja .
* Daraja ya pili ni kufunga siku ya tisa na kumi .
* Daraja ya tatu ni kufunga siku ya kumi peke yake.

Na sababu ya ikhtilafu hiyo imetokana na ikhtilafu ya mapokezi .

Na iliyo na nguvu miongoni mwa athari hizo ni hii inayofuata; Imepokewa kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) yakwamba amesema: "Fungeni siku ya tisa na ya kumi, wakhalifuni Mayahudi.

Amesema muandishi katika kitabu cha "*Rawdhwatun– Naadiya*" wako juu ya neno hilo wanavyuoni na wanaona ni sunnah wengi wao kufunga siku ya tisa na ya kumi.

Na ni makuruhu kufunga siku ya 'Ashura peke yake.

Amesema al-Haafidh katika Fat-h: "Neno la Mtume (صلى الله عليه وسلم): "*Nikiishi mpaka mwaka ujao nitafunga siku ya tisa.*" Neno hilo ni wazi kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akifunga siku ya kumi na akakusudia kufunga siku ya tisa ,akafa kabla ya hapo. Kisha hivyo alivyo kusudia katika kufunga hiyo siku inawezekana maana yake kwamba yeye hatafunga siku hiyo tu bali ataongezea na siku ya kumi.

Na ima ni kuwakhalifu Mayahudi na Manaswara na hili ndilo lenye nguvu zaidi. Na kwa neno hili, baadhi ya mapokezi ya Muslim hufahamisha hivi na kwa hiyo, alipoulizwa Imaam Ahmad ibn Hanbal Imaam mtukufu wa Sunnah kuhusu saumu ya 'Ashura alisema: "Afunge mtu siku ya tisa na siku ya kumi." Na madhumuni ya maneno ya Imaam Ahmad ni kwamba ni makuruhu kufunga siku ya kumi peke yake . Kwa sababu yeye aliulizwa saumu ya siku hiyo akafutu kwa kufunga siku mbili (ya Tisa na ya Kumi). Na akaamrisha hivyo na akaja'alia hii kuwa ndiyo Sunnah kwa anayetaka kufunga 'Ashura na aliifuata Imaam Ahmad hadeeth hiyo ya ibn 'Abbaas. Na ibn 'Abbaas alichukia kufunga siku ya kumi pekee juu ya ilivyo mashuhuri kwake.

UZUSHI KATIKA SIKU HII

Amenakili *Al Munawi* kutokana na Al *Majdi lughawi* kwamba yeye amesema mambo yanayopokewa katika fadhla za Saumu ya siku ya 'Ashura na kuswali ndani yake na kutoa chakula na kujipaka hina na kujipaka mafuta na kujitia wanja; yote hayo ni uzushi yaliozushwa na aliye muuwa Hussein (رضي الله عنه).

UZINDUSHI

Amma hadeeth inayosema "*Mwenye kupika vyakula vingi kwa ajili ya nafsi yake na watu wake siku ya 'Ashura Allaah humkundulia kwa mwaka mzima.*" Hadeeth hii ni dhaifu kwa njia zake zote. Na kuhakikisha maneno hayo ni katika kitabu cha *Tamaam ul-Minna* cha Sheikh Albaani (رحمه الله)

Amesema Sheikh Ul-Islaam ibn Taymiyyah (رحمه الله): "Na amekuwa Sheitwaan kwa sababu ya kuuwawa Hussein (رضي الله عنه) anawazushia watu bid'a aina mbili. Uzushi wa kuhuzunika na kuomboleza siku ya 'Ashura , katika kujipiga makonde na kupiga makelele na kulia na kuimba na... na kuwaimbia walio kufa na kuwatukana ma-Salaf (watu wema waliotangulia), na kuwalaani, na hata kutukanwa Maswahaba na husomwa habari za kuuwawa kwa Hussein ambazo nyingi ni urongo na ilikuwa makusidio ya mwenye kufanya hivyo ni kuleta fitna na mfarakano baina ya umma, kwani jambo hili si wajibu wala si Sunnah kwa mapatano ya waislamu ispokuwa ni kuzusha huzuni , na kuomboleza katika misiba ya zamani ni katika madhambi makubwa aliyo yaharamisha Allaah.

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

MWEZI WA MUHARRAM

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Na vilevile uzushi wa furaha na walikuwepo huko mji wa Al-Kufa Mashi'ah wenye kumnusuru Hussein na alikuwa mkubwa wao ni Al-Mukhtaar ibn 'Ubbeyd mrongo na walikuwepo watu wenye kumchukia Ali na watoto wake na katika hao ni Al-Hajaj ibn Yusuf Ath-Thaqafee na imethubutu katika Swaheeh kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema atakuwepo katika kabila la ath-Thaqafee mtu mrongo, Mubiir na akawa ni huyo Mshi'ah ndiye mrongo, na huyo naswibu ndio Mubiir, hao wakazusha huzuni na hawa wakazusha furaha. Na uzushi huu asili yake unatokana na wabaguzi wabatili juu ya Hussein na kila uzushi ni upotevu. Na hakusunisha yeyote katika maimamu na wengineo sio kuhuzunika wala kufurahia wala halina lolote katika hayo hoja ya kisheria mpaka aliposema sheikhul Islam ibn Taymiyyah (رحمه الله) na hakuna shaka kwamba kumuuwa Hussein ni katika madhambi makubwa lakini kuuwawa kwake si jambo kubwa sana kuliko kuuwawa walio bora zaidi kuliko yeye ambao ni Mitume na Maswahaba wa kwanza walio tangulia na Maswahaba waliouwawa katika vita vya Uhud na walio uwawa katika kisima cha Mauna na kama kuuwawa kwa 'Uthmaan na kuuwawa kwa Ali. Na ametaja ibn Taymiyyah (رحمه الله) huko nyuma kwamba jambo la wajibu wakati wa kupata msiba ni kusubiri na kusema "hakika sisi ni wa Allaah, na kwake yeye tutarejea (atatupa jaza yake)" kama anavyopenda Allaah na Mtume wake.

MAANA YA 'ILMU Sheikh Ibn Ul-'Uthaymeen

'Ilmu ki-lugha ni kinyume cha Ujinga na kujua kitu kama kilivyo, kujua kwa kukatikiwa.

Amma ki-Istilaahi, kwa hakika wamesema baadhi ya Wanavyuoni; ni maarifa, nayo ni kinyume cha Ujinga. Wengine wakasema katika wanavyuoni: Hakika 'ilmu ni wazi zaidi kujulikana.

Na yanayotuhusu (katika mlango wa 'ilmu) ni 'ilmu ya ki-shari'ah (ya ki-Islamu) na makusudio ya ('ilmu Shar'ee) ni: 'ilmu ya kujua mambo ambayo alomteremshiya Allaah Mtume wake katika Hoja na Uongofu. Kwahivyo l'ilmi iliyosifiwa ni 'ilmu ya wahyi, 'ilmu ya kumjua Allaah. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Allaah akimtakia kheri mja humpa ufahamu katika Dini."* Na akasema: *"Hakika manabii hawakurithi Dinari wala Dirham, kwa hakika si jengine walilolirithi isipokuwa ni 'ilmu; atakaechukuwa basi atachukuwa fungu kubwa."*

Na inajulikana kuwa kile walichorithi manabii ni 'ilmu ya Sheriya ya Allaah na wala sio nyengine, kwani Manabii (عليهم السلام) hawakurithisha watu 'ilmu za ki-Ufundi na yanayohusiana nayo.

Kwahiyo 'ilmu ya Shari'ah ya ki-Islamu ndiyo ile ambayo husifiwa alonayo, lakini mimi pamoja na hilo sikatai kuwepo na faida katika 'ilmu nyengine; lakini hiyo faida kwa njia mbili zikisaidia katika twa'a ya Allaah na kunusuri Dini yake na wakanufaika nayo waja wa Allaah, litakuwa hilo ni kheri na maslaha, na inawezekana kuzisoma ('ilmu nyengine). Ni waajib katika baadhi ya hali ikiwa itaingia katika neno la Aliyetukuka: **"Basi waandalieni (wawekeeni tayari) nguvu mziwezao (silaha) na Mafarasi yaliyofungwa."**

Na wametaja wanavyuoni wengi yakwamba kusomea 'ilmu za ufundi na ta'aluma ni (*fardhi kifaayah*). Na hilo ni kwa kuwa watu ni lazima wapate chombo watakachopikia ndani yake, na kunywea ndani, na yasiyokuwa katika mambo wanayonufaika nayo, kusipopatikana wa kutengeza vyombo hivi itakuwa kusoma kwake ni fardh kifaayah. Na nahapa wamekhitilafiana wanavyuoni, na kwa hali yoyote ningependa kusema; "Hakika 'ilmu ambayo imesifiwa ni 'ilmu ya Dini ambayo ni kukifahamu kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume wake (صلى الله عليه وسلم) . Kinyume cha hayo ni emma iwe njia ya kupelekea kheri au kupelekea shari, kwahiyo Hukmu yake ni kulingana na kinachopelekea."

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 4)

akasema: "Kamba ya Allaah" imefasiriwa kuwa; Kitabu Chake, Dini Yake, Uislamu, Dhati, Amri Yake, Agano Lake, Utiifu kwa Allah, na Jamaa'ah. Misemo yote haya yametajwa na maswahaba na wale waliowafuata katika kutenda mema mpaka siku ya Kiyama. Na yote haya ni Swaheeh, kwani Qur'aan inatuamrisha juu ya Dini ya Uislamu - na hii ndiyo Amri ya Allaah, (vile vile ndilo) Agano lake na Utiifu wa Mola. Na kushikamana na yote haya kwa ujumla (kwa umoja wa watu) haitawezekana isipokuwa kwa Jamaa'ah. Na dini ya Uislamu ki uhakika na kuwa mkweli na wazi kwa Allaah. Ibn Jareer at-Tabaree amesema katika tafseer yake kuwa Qataada amesema kuhusu aya hii "Wala musifarikiane, na mukumbuke baraka ya Allaah juu yenu" - Kwa hakika, Allaah anachukia kuona kuwa ummah umegawanyika na Anatukataza na jambo hili. Na anapenda kuona tunatwi'i na kushikamana na Jamaa'ah. Basi pendaneni baina yenu kwa yale Allaah anayowapendelea - kiasi cha uwezo wenu. Na hamna nguvu isipokuwa kwa (amri yake) Allaah.

WAJIBU WA KUSHIKAMANA NA JAMAA'AH Mtayarishi: Sheikh Ibn Burjis

Kuna maafikiano makubwa baina ya Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah kuwa ni wajibu wetu kushikamana na Jamaa'ah na kuwa imekatazwa kujitenga nayo; Kushikamana na Jamaa'ah ni jambo jema na kujiepusha na kujitenga nayo ni ufisadi.

Kuna dalili nyingi kutoka katika Qur'aan na Sunnah ambayo imetaja kuhusu jambo hili, mpaka kufikilia kiwango cha kuwa tawaatur. Vile vile kuna riwaya chungu nzima kutoka kwa ma-Salaf (watangulizi wetu wema) kuhusiana na haya. Allaah (سبحانه وتعالى) Akasema: **"Na mushikamane na Kamba ya Allaah, nyote kwa pamoja, wale musifarikiane"** (Surat- Aal-Imraan 3:103)

Ibn Abee Haatim amesema: "Babangu alinieleza kuwa: Amr Ibn 'Alee As-Sairafee alinieleza, akisema: Abdu Rabbih Ibn Baariq al-Hanafee - na akamsifu kwa uzuri - kuwa alinihadithia na kusema: Simaak Ibn al-Waleed al-Hanafee amesema yakuwa alikutana na Ibn 'Abbaas mjini al-Madinah na akamwambia:"Wasemaje kuhusu huyu kiongozi wetu anayetutawala, na kutunyanyasa (kutudhulumu na kutukandamiza) na kutushtumu, jee ni kwa nini basi tusimzuie (yaani tumpige vita na kumpinga)?"

Ibn Abbaas akamjibu:"Laa! bali mumtwi'i, Ewe Hanafee". Na akaendelea kusema: "Ewe Hanafee, (shikamana na) Jamaa'ah, Jamaa'ah! Kwa hakika mataifa yaliowatangulia waliangamizwa kwa ajili ya kujigawanya (kufarikiana wao kwa wao). Jee hukusikia Allaah aliposema: **"Na mushikamane na Kamba ya Allaah, nyote kwa pamoja, wala musifarikiane...."**

Amesema Ibn 'Atiyyah katika tafseer yake, "Rai za wanavyuoni wa tafseer zimetofautiana kuhusu maana ya hii sehemu ya ayah "Kamba ya Allaah". Basi Ibn Mas'ood akasema "Kamba ya Allaah (ina maanisha) ni Jamaa'ah". Anas Ibn Malik anatueleza kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Kwa hakika banu Israeel waligawanyika mapote sabiini na moja . Ummah wangu utagawanyika mapote sabiini na mbili - yote hayo ni yenye kuangamia katika (moto wa) Jahannam isipokuwa moja. (Maswahaba) wakamuuliza:"Ewe mjumbe wa Allaah, ni kundi gani litakalo okoka?" Naye akakunja ngumi na kusema;"Jamaa'ah", halafu akawasomea aya **"Na mushikamane na Kamba ya Allaah, nyote kwa pamoja"**.

Ibn Mas'ood alisema katika moja ya khutbah zake:"Nyinyi nyote kwa ujumla, munawajibika kuwa watiifu (kwa Allah) pamoja na Jamaa'ah, kwani hii ndiyo Kamba ya Allah aliotuamrisha sisi Mola wetu." Qataada naye akasema:"Kamba ya Allah ambayo Ametuamrisha tushikamane nayo ni Qur'aan". Nae As-Suddee akasema: "Maana ya Kamba ya Allah ni kitabu chake Allaah". Ibn Mas'ood na Ad-Dahhaak pia walisema hivyo. Na mengine mengi pia yalisemwa ambayo yamefanana na haya (katika misemo iliotangulia).

Neno "jamee'an" (nyote kwa pamoja) imeungana na amri " 'l'tasimoo" (shikamaneni), basi maana yake itakuwa "muwe wamoja juu ya kushikamana na hiyo Kamba ya Allah". Na "musifarikiane" ina lenga aina ya migawanyo ambayo haitawafanya mushiriki katika Jihaad na mambo ya kulinda dini na Neno la Allaah. Huu ndiwo mgawanyiko uliotokamana na fitna na kutokubaliana katika mambo ya imani." [mwisho wa maneno ya Ibn 'Atiyyah]

Nami nasema kuwa, kutofautiana katika tafseer ya "Kamba ya Allah" ni tofauti inayo tuashiria aina nyingi ya maana ya neno hilo, wala sio tofauti ya maana halisi ya neno hilo, kama tulivyoelezwa na Ibn 'Atiyyah, Ibn 'Abdil-Barr na muhaqqiqeen wengineo. Na maoni yake kuwa (Kamba ya Allaah) inamaanisha Kitabu chake inakusanya misemo yote ya salaf.

Al Qurtubee alitaja katika tafseer yake, rai ya wale wanaosema "Kamba ya Allah" inamaanisha Qur'aan, na rai ya wale wanaosema kuwa inamaanisha Jamaa'ah. Kisha akasema: "Maana iliyokusudiwa hapa zimekaribiana na zimefanana kwani Allaah anatuamrisha tuwe wamoja na kutukataza na kufarikiana. Hii ni kuwa (huko) kufarikiana ni maangamizi na kushirikiana na Jamaa'ah ni maokovu. Naye Shaykhul Islaam ibn Taymiyyah

KILIFI BOOKS & STATIONERY STORE LTD

Executive Director: Muhammad A. Said

Suppliers of: *School Textbooks & Stationeries, Office Stationeries, Films, Dealers of AirTel Cards and Safaricom Cards.*

* Madrasatul Munawwar Wakf Building—Mombasa
* Jamo Kenyatta Avenue—Mombasa
* Hospital Street—Opposite P.H.D Mombasa.

P.O.Box 99900 *Tel: 041-2495763*

Postal Code: 80107 *Fax: 041-2495764*

E-mail:kilifibks@africaonline.co.ke *Mobile: 0722-265103 / 0722-669414*